

FORM 2 TERM 1 2021

KISWAHILI

1. Ufahamu. (alama 10)
Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

MWANAMKE

Jogoo anapowika, ana jambo atangaza,
Atangaza kuamka, limeshatanduka giza,
Giza limeshaondoka, uache kujiduwaza,
Mwanamke amka!

Jogoo anapowika, mwanamke amjuza,
Amjuza kuamka, amulikwe na mwangaza,
Mwangaza umeshafika, aache kujilegeza,
Mwanamke amka!

Jogoo anapowika, mwanamke ahimiza,
Ahimiza kutimka, mbio ili kujikuza,
Kujikuza si dhihaka, elimu kuitukuza,
Mwanamke amka!

Joogoo anapowika, mwanamke amkuza,
Amkuza kuzizika, tamaduni za kuviza
Kuziviza kwa haraka, mila zinazopumbaza,
Mwanamke amka!

Jogoo anapowika, mwamke atukuza,
Atukuza amefika, kupokea yake tuza,
Tuza ya kurevuka, muamko kutangaza,
Mwanamke amka!

Jogoo anapowika, mwanamke akataza,
Akataza kutotaka, minyanyaso ya kuliza,
Kuliza na kuudhika, hakiye kugandamiza,
Mwanamke amka!

Jogoo anapowika, mwanamke amwongoza,
Amwongoza umefika, muda wa kuongoza,
Kuongoza kwa hakika, umma pasi kujitweza,
Mwanamke amka!

Tamati jogoo wika, mwanamke azoweza
Azoweza kurauka, kwa bidii kujikaza,
Kujikaza na kutoka, jikoni kulomviza,
Mwanamke amka!

MASWALI

- a) Lipe shairi kichwa kingine mwafaka. (al 2)
- b) Ni ujumbe upi anaoutoa jogoo kila anapowika? (al 4)
- c) Eleza maana ya neno ‘amka’ kwa mujibu wa maudhui ya shairi. (al 1)
- d) Onyesha mpangilio wa yina na mizani katika shairi. (al 2)
- e) Eleza aina ya shairi kwa kuzingatia idadi ya mishororo. (al 1)

MATUMIZI YALUGHA (AL 15)

- a) Tambua viambishi awali katika maneno uliyopewa. (al 2)
i) Mgeni

ii) Kikapu
- b) Andika sentensi zifuatazo ukitoa kinyume cha maneno yaliyopigwa mstari. (al 2)
i) Alipokuwa akienda kulala usiku aliushindika mlango wa nyumba yake.

ii) Kabla ya kwenda kazini asubuhi alikuwa tayari ameshawaelewa.
- c) Kanusha sentensi zifuatazo. (al 3)
i) Mtoto anapoanguka hulia.

- ii) Ningalifanya kazi ningalikuwa tajiri.
 - iii) Amekuwa akifanya kazi kwa bidii.
- d) Tambua aina za sentensi zifuatazo (al 2)
- i) Mwanafunzi anasoma hadithi.
- ii) Mtoto atakula kwanza kisha aende akacheze.
- e) Eleza maana ya misemo ifuatayo. (al 2)
- i) Kuona haya
- ii) Kutia chumvi
- f) Jaza kihuishi mwafaka katika sentensi zifuatazo. (al 2)
- i) Maarusi walifuatia kasisi hadi kanisani.
- ii) kuja waingereza Africa ilikuwa huru.
9. Tumia kiunganishi mwafaka kujaza pengo. (al 2)
- i) Alikuwa na kazi nyingi, alikuja kuniona.
 - ii) Umefika mapema, tuanze shughuli zetu saa hii.

ISIMU JAMII (AL 15)

Fafanua sifa tano za sajili ya kituo cha matibabu.

i)

ii)

iii)

iv)

v)